SwahiliWeb

ELECTRONIC DEPOSITORY AND RESOURCE ARCHIVE

www.swahiliweb.net

Archive: Pat Caplan

Document: Mgeni binti Nassor

File reference: SW/PC/13014

This document has been downloaded from the SwahiliWeb archive on the understanding that it is copyright under the laws of the United Kingdom and the Berne Convention, and that no further copying, storage or distribution, in any form or by any means, including electronically, is permitted except under the provisions of fair dealing.

Copyright of all materials deposited with SwahiliWeb remains with the copyright holder. Those seeking copyright and associated permissions will be referred to the copyright holder.

**Mgeni binti Nassor 1985 interview,**
**transcribed Dec. 2010 by Joseph Bwathondi**

*I had known Mgeni since she was a child at the time of my first visit to Kanga. At the time of this conversation, she was probably in her thirties and married to her second husband. She is the subject of my article 'In my office we don't have closing hours' (1995)*

PAT: Sasa utaenda nae bure? Au utapewa zawadi?

MN: Bure huendi mpaka zipatikane pesa.

PAT: Kama kiasi gani hivi.

MN: Atakazozitoa kama 100, 200.

PAT: Vitu vingine kama shanga bangili?

MN: Nguo atakupa

PAT: Hivyo. Sasa katika ili majambo vile wanavyofanya bwana na bibi, wakikaa pamoja na watoto wao itakuwaje? Si Watoto watajua mambo yote au wanatafanya watoto wakishalala ? manake wengine wanakaa kwenye nyumba ndogondogo, chumba kimoja mama baba na watoto. Sasa wakitaka kufanya mambo zao itakuwaje?

MN: Wanalala? Wanasubiri watoto wakishalala ndio tena wanafanya mambo yale

PAT: Sasa inakuaje? Anakuwa kama anaanza baba au anaanza mama?

MN: Siku nyingine anaanza mama na siku nyingine anaanza baba.

PAT: Ndio hata na sie tunafanya hivyo hivyo. Lakini siku zote baba anapanda juu ya mama au vipi?

MN: Utakavyo.

PAT: Utakavyo

MN: Ikiwa kupanda wewe kwa baba au ikiwa kupandwa wewe na baba sawa tu. Nyie mnafanya ushirika?

PAT: Aah! Utakavyo. Na mume kumuuingilia kwa nyuma anaweza?

MN: Ndio.

PAT: Anafanyaje?

MS : Anakuingilia tu lakini kule kunakotoka mavi ndio kubaya.

PAT: Sio hivyo.

 ©Pat Caplan 2013

MN: Yaani kwa kukaa kwa nyuma hii inawezekana.

PAT: Kuzuri? Unakumbuka?

MN: Ndio.

PAT: Lakini hapa desturi ya kugusa gusa kwa mdomo ipo?

MN: Ndio ipo, huku midomoni , masikioni na puani ipo. Yanafanyika yote

PAT: Lakini hapa desturi za mwanamume anayempenda mwanamume mwenzake hipo.

MN: Hakuna, kufanya mwanamume kwa mwanamume?

PAT: Eeh

MN: Hakuna

PAT: Lakini nimesikia pande za Unguja wanafanya

MN: huko wanafanya.

PAT: Na wanawake kwa wanawake wanafanya

MN: Wanawake kwa wanawake hapana. Labda huko huko. Wala sijawahi kusikia.

PAT: Wewe unasemaje?

MN: Mwanamke kwa mwanamke?

PAT: Mmh!

MN: Wanaona uzuri gani?

PAT: Sijui? Hakuna, ni kweli.

MN: Mwanaume atakushika huku na kule mwenyewe utasikia raha na sio mwanamke mwenzako.

PAT: Sasa mwisho wake inakuwaje? Unaposikia utamu kuliko

MN: Kule unapokojoa ndio utamu wenyewe.

PAT: Sasa tuseme ile damu inayotoka kila mwezi, kama inashika mimba haitoki sasa inafanya nini mule ndani?

MN: Sasa inakaa tu kwa sababu za kimungu mungu.

PAT: Mpaka mimba inakwisha halafu inaanza tena. Na mtoto akiwa ndani kwenye mimba anapata roho yake lini?

 ©Pat Caplan 2013

MN: Roho yake kupata mtoto mpaka siku ya kuzaliwa

PAT: Ndio apate roho?

MN: Ndio manake alikuwa ndani na roho atapata akitoka nje?

PAT: Sasa ikiwa bahati mbaya  baada ya miezi sita akiwa tumboni mimba ikaaribika je utamzika?

MN: Ndio

PAT: Kama mtu mzima.

MN: Ndio

PAT: Ikiwa ndogo ndogo kama miezi mitatu?

MN: Tutazika.Ili mradi itatoka damu tutamzika.

PAT: Tuseme mwanamke ameshika mimba na yeye  hataki kuzaa, hawezi kutumia dawa au kufanya kitu chochote hasipate? Sasa mtafanya nini hapa?

MN: Huku siku hizi kuna majira?

PAT: Halafu inatoka?

MN: Ndio.

PAT: Wengi wanafanya hivyo?

MN: Ndio wanafanya

PAT: Kwa sababu wamechoka kuzaa. Mpaka na mtoto akishika mimba anaweza kufanya hivyo?

MN: Eeh! Kama hautaki kuzaa.

PAT: Sasa atapata wapi mwingine?

MN: Wapo tele

PAT: Majira ndio ina maana gani?

MN: Ni dawa

PAT: Ni dawa ya miti?

MN: Hapana ni ya hospitali.

PAT: Lakini hii ni ya kuzuia

MN: Kuzuia uzazi

 ©Pat Caplan 2013

PAT: Lakini ukishapata  mimba utafanyaje?

MN: Ukishapata mimba?

PAT: Ndio.

MS :Itabidi unywe dawa za miti.

PAT: Unakunjwa dawa za miti na unaambiwa itatoka/kuaribika?

MN: Kama mimba ya miezi miwili mitatu unaweza.

PAT: Ikishakuwa kubwa basi hauwezi?

MN: Ndio manake itatoka na Roho yako weye.

PAT: Sawa. Lakini kule hospitali operation hawafanyi?

MN: Operatio?

PAT: Ya kukata mimba hawafanyi. Sasa wewe uliniambia watoto wanne wazuri.

MN: Ndio.

PAT: Wawili unaona wachache.

MN: Ukiwa nao wane unaweza kupata wawili wanaume wawili wanawake na pindi unapopata matatizo ya kiafya na kadhalika watakushughulikia. Sasa watoto wawili tu wao wafanyeje?

PAT: Sijuhi?

PAT: Lakini ukizaa kila mwaka mpaka watoto 10 na zaidi si nzuri

MN: Ndio .

PAT: Wewe hakutaka. Unaangaika.

MN: Kweli.

PAT: Lakini hapa wanazaa wengi sana  je wanazaa kwa sababu wanataka au ni hivi hivi tu?

MN: Mie nilipata mimba tisa na wengine walikufa .

PAT: Wengine wamekufa?

MN: Ndio

PAT: Wadogo wadogo

MN: Ndio.

 ©Pat Caplan 2013

PAT: Sasa ungelikuwa na hao tisa ingekuwaje?

MN: Ningekuwa nao. Yule ananiendea maji Yule anafanya shughuli hizi basi ni kama hivyo (yaani wengefanya kazi mbali mbali)

PAT: Si vibaya.

PAT: Sasa katika wale watoto tisa wanne wamepotea. Katika mimba au

MN: Wote nimezaa. Wengine walikaa mpaka siku 40 lakini ndio bahati mbaya tena

PAT: Ulizaa na huyu mume wa kwanza au wa pili

MN: Wakwanza.

PAT: Wakwanza. Sawa

PAT: Sasa kuna makabila mengine yanasema kwamba mwanamke akishapata mtoto harusiwi kulala na mumewe mpaka mtoto afikishe miaka miwili, hapa hakuna kitu kama hicho?

MN: Bara huku ndio hivyo

PAT: Ikishaisha 40 tu unaruhusiwa

MN: Sikukazwa mpaka miaka 2.

PAT: Hata mie Sikuweza

MN: Miaka miwili sikuweza.

PAT: Watoto wanakusaidia katika maisha yako?

MN: Ndio wananisaidia.

PAT: Kivipi?

MN: Wananitumia nguo chakula. Nguo hii katoa mtoto hii katoa mtoto nah ii katoa mtoto.

PAT: Watoto wa kiume tu au na wakike?

MN: Wakike, wakike, wanaume wao wanatuma chakula na kitoweo

PAT: Sasa kama mwanamke hajazaa mtoto sasa atafanya nini akiwa mzee?

MN: Haa !atapata riziki yake kupitia kwa watoto wa ndugu

PAT: Ndugu zake.

MN: Watamsaidia

 ©Pat Caplan 2013

PAT: Sasa wewe unaonaje mwanamke ambaye hawezi kuzaa? Ataona uchungu au vipi?

MN: Ataona, wanandugu watamuonea uchungu.

PAT: Atakwenda kwa waganga

MN: Mmh!

PAT: Wa watoto?

MN: Mmmh!

PAT: Kuna dawa maalum?

MN: Ya kupata mtoto?

PAT: Ndio.

MN: Mtoto ni mwenywe mungu hakuna dawa yoyote


©Pat Caplan 2013